JINA:………………………………………..…. SHULE…………………………………………

NAMBARI YA USAJILI……………….………TAREHE:……….…….SAHIHI………………

**102/3**
**KISWAHILI (Fasihi)**
**KARATASI YA TATU**
**KIDATO CHA NNE**
**MUDA: 2½**

# TATHMINI YA DAYOSISI YA KAKAMEGA
# MTIHANI WA JULAI/AGOSTI

**MAAGIZO**

a) Andika jina lako, nambari ya usajili, mkondo, jina la shule katika nafasi ulizoachiwa hapo juu
b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe katika nafasi ulizoachiwa hapo juu
c) Jibu maswali **Manne** pekee
d) Swali la kwanza ni la **lazima**
e) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu zingine zilizobaki yaani, Riwaya, Tamthilia, Hadithi fupi na Fasihi simulizi.
f) Usijibu maswali **mawili** kutoka sehemu moja

## Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| JUMLA | 80 | |

## SEHEMU A: USHAIRI

1. **LAZIMA**

**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Daima alfajiri na mapema
Hunipita na jembe na kotama
Katika njia iendayo Kondeni
Kama walivyofanya babuze zamani;
Nimuonapo huwa anatabasamu
Kama mtu aliye na kubwa hamu
Kushika mpini na kutokwa jasho
Ili kujikimu kupata malisho

Anapotembea anasikiliza
Videge vya anga vinavyotuimbiza
Utadhani huwa vimengojea
Kwa usiku kucha kuja kumwimbia;
Pia pepo baridi kumpepea
Rihi ya maua zikimletea
Nao umande kumbusu miguu;
Na miti yote hujipinda migongo;
Na yeye kuendelea kwa furaha
Kuliko yeyote ninayemjua
Akichekelea ha ha ha ha ha…

Na mimi kubaki kujiuliza
Kuna siri gani inayomliza?
Au ni kujua au kutojua?
Furaha ya mtu ni furaha gani
Katika dunia inayomhini?
Ukali wa jua wamnyima zao
Soko la dunia lamkaba koo;
Dini za kudhani zamsonya roho
Ayalimia matumbo ya waroho;
Kuna jambo gani linamridhisha?
Kama si kujua ni kutokujua
Laiti angalijua, laiti angalijua!

**MASWALI**

a) Eleza hali ya mzungumzaji katika shairi hili. (alama 3)
b) Huku ukitoa mifano, onyesha aina mbili za uhuru wa kishairi uliotumiwa katika shairi hili. (alama 2)
c) Fafanua aina mbili za taswira ukirejelea ubeti wa pili. (alama 2)
d) Bainisha vipengele viwili vya kimtindo katika shairi hili. (alama 2)
e) Bainisha aina mbili za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 2)
f) Eleza toni ya shairi hili. (alama 2)
g) Tambua nafsineni katika shairi hili. (alama 1)
h) Eleza muundo wa shairi hili. (alama 2)
i) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha nathari. (alama 4)

## SEHEMU B: RIWAYA

A. Matei-Chozi La Heri

Jibu swali la 2 au la 3

2. **"Dickson wewe jikaze. Mzee wako hayupo hapa….."**
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   b) Bainisha hali inayorejelewa ambayo ilimhitaji mhusika huyu kujikaza. (alama 2)
   c) Jadili mikakati ambayo mrejelewa alitumia kukabiliana na hali yake. (alama 6)
   d) Eleza umuhimu wa mandhari yanayorejelewa katika dondoo hili. (alama 8)
3. **Changanua mtindo katika dondoo lifuatalo.** (alama 6)
   a)

Lakini kumbuka mtu huenda msalani baada ya shibe! Tumbo shinda hata haja ndogo haliendi! Ugenini humu hamkuwa na mashamba. Waliokuwa wamebahatika kwa kubeba nafaka haba walizotoa zikatumiwa kwa ujima. Sasa matumbo yalianza kudai haki hata baada ya kujua kuwa haki yenyewe haikuwa mikononi mwetu. Haki ilikuwa mikononi mwa walio na nguvu ambao ndio waliotufanya kuwa wageni wa pori. Vilio vya watoto wenye njaa vilianza kusikika. Polepole vilio hivi vilianza kupungua, njaa na ugonjwa vimefanya kazi. Nilianza kufikiria kuwa hali ikiendelea hivi tutaipungia dunia mkono.

   b) "Wakati mwingine tunashiriki katika njama zao chafu za kifisadi, tunawasaidia vikongwe wasiojua kusoma na kuandika…..afaaye! mama unataka KIBOKO, au PAPA?
      i. Tambua swala linalodokezwa katika kauli hii. (alama 2)
      ii. Wanaorejelewa katika kauli hii, wamechangia kurudisha nyuma maendeleo ya jamii kwa njia mbalimbali. Fafanua. (alama 12)

## SEHEMU C: TAMTHILIA

Timothy M. Arege: Bembea ya Maisha

Jibu swali la 4 au la 5.

4. "Ndivyo…ndivyo…hayakuishia hapo. Baada ya ile mvua ya baraka iliyowanyea, watu walianza tena kuwasema kuwa hawana mtoto wa kiume."
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   b) Tambua mbinu mbili za kimtindo katika dondoo hili. (alama 2)
   c) Fafanua umuhimu wa msemaji katika kuijenga tamthilia hii. (alama 4)
   d) Eleza sifa mbili za msemaji wa kauli hii. (alama 2)
   e) Kwa kutolea mifano, onyesha jinsi mwandishi alivyoshughulikia maudhi ya utamaduni wa kale katika tamthilia hii. (alama 8)
5. 
   a) Jadili changamoto zinazokumba asasi ya ndoa kwa mujibu wa tamthilia ya Bembea ya Maisha. (alama 8)
   b) Asna na Sara ni wahusika wawili wenye mitazamo tofauti kuhusu maisha. Thibitisha. (alama 6)
   c) Changanua mtindo katika dondoo hili. (alama 6)
      Ukilazwa tayari unakuwa umeonja seli. Hata wenyewe hawana mlahaka mwema. Amri na vitisho kama askari. Unashindwa kama uuguze moyo ama ugonjwa. Katika wodi hewa iliyojaa harufu ya dawa imezagaa, vitanda vimesalimu amri mpaka shiti zikagura. Yaani hali nzima haikupi matumaini ya kutoka ukiwa bora.

## SEHEMU D: HADITHI FUPI

D.W Lutomia na P. Muthama

Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine.

Jibu swali la 6 au 7

6. **Wanawake wanafaa kujilaumu kwa kudhalilishwa na jamii. Thibitisha kauli hii kwa kurejelea hadithi zifuatazo:**
   i. Fadhili za Punda. (alama 10)
   ii. Kifo cha Suluhu. (alama 10)

7. **Rayya Timammy: Ahadi ni Deni.**

a) Changanua mtindo katika dondoo hili. (alama 6)

Maneno hayo yalikua kama hirizi aliyoamua kuivaa ili yamwongoze na aliamua hilo akijiambia kimoyomoyo kuwa ingawa babake hayupo tena; hata huo mwaka haukufika nusu alipata tena habari mbaya… mwalimu mkuu alimwita afisini siku hiyo kutoka darasani…Alipofika afisini mwa mwalimu mkuu, mwalimu mkuu aliweza kusoma wahaka usoni mwake. Akanena naye kwa upole…Aliona kuwa shule yake ingefanya vyema sana kama wasichana wote wangekuwa…kwa vitendo!

b) Bainisha mbinu mbili zinazoweza kutumiwa kutambua sifa za mrejelewa wa maneno haya. (alama 2)

c) "Likizo ilipoisha alirudi kwanza kidato cha pili lakini moyo ulikuwa mzito. Jambo lilompa ari ya kufanya hivyo ni yale mazungumzo ya mwisho na babake."

i. Tambua suala linalodokezwa katika kauli hii. (alama 2)

ii. Fafanua sifa mbili za mrejelewa katika kauli hii. (alama 2)

iii. Suala ulilotaja hapo juu (i) limekumbwa na changamoto mbalimbali katika hadithi hii. Fafanua. (alama 8)

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

8. **Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.**

Hapo zamani za kale paliishi mtoto katika kisima kimoja. Siku moja mtoto huyu aliokota kijiwe karibu na soko kuu. Kijiwe kilikuwa kikimeremeta kwa rangi mbalimbali na kilizingirwa na pete ya dhahabu.

Mtoto huyu na wenzake walianza kurushiana kijiwe hicho. Baada ya muda kilianza kuongezeka umbo na kuonekana kama kiwiliwili cha binadamu. Kikaanza kuwakimbiza wale watoto. Kutokana na ukelele wao watu walikuja kutazama nini kilikuwa cha mno. Walipofika walikutana ana kwa ana na dubwana hilo. Lilizidi kuongezeka umbo na likawameza wote pamoja na mifugo wao. Wachache waliojaribu kukimbia liliwashika kwa mikono yake mipana na mirefu. Kwa bahati njema alikuwepo mama mmoja aliyeona haya yote. Alikuwa mbali na hapo. Aliteremka kutoka kilele cha mlima na kuwapata wakulima makondeni na sawia akawajuza kuhusu kitendo kilichomwogofya sana. Wote wakaacha shughuli zao na wakatwaa silaha zao wakaelekea soko kuu.

Dude sasa lilikuwa limejilaza baada ya shibe, wakulima wale walichagua watu sita ambao walijulikana kwa ushujaa wao. Pamoja walilinyemelea lile nyangarika na kulikata mara moja. Lilitoa mkoromo mkuu kabla halijakata kamba. Punde, wanakijiji kwa uangalifu mkubwa walitoboa tumbo lake wakitarajia kupata maiti za wapenzi wao pamoja na mifugo wao. Wote walijawa na furaha kuu walipoona wapenzi wao wakijichomoza kutoka tumboni, mmoja baada ya mwingine hadi akatoka yule wa mwisho. Mbuzi, kondoo na ng'ombe wote walitoka mmoja mmoja.

Siku hiyo kuliandaliwa sherehe ya kumshukuru Muumba kwa wema wake. Watoto walishauriwa wasithubutu kuchezea vitu wasivyovijua.

**MASWALI.**

a) Bainisha kipera cha utungo huu. (alama 1)

b) Eleza mambo matatu yanayoonyesha kwamba kipera hiki ni sanaa. (alama 3)

c) Tambua mifano miwili ya fantasia katika hadithi hii. (alama 2)

d) Unakusudia kutumia mbinu ya kushiriki kufanya utafiti kuhusu tungo za aina hii. Eleza manufaa manne ya mbinu hii. (alama 4)

e) Fafanua mikakati sita ambayo jamii inaweza kutumia ili kuudumisha utanzu huu. (alama 6)

f) Bainisha shughuli mbili za kiuchumi na mbili za kijamii zinazoendelezwa na jamii inayojawiriwa katika utungo huu. (alama 4)